# Muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva katika Kuhamasisha Usomaji Nchini Tanzania

*S. Omari*

**Ikisiri**

Usomaji ni suala muhimu kwa kila jamii ili kujiletea maendeleo katika nyanja mbalimbali. Muziki wa kizazi kipya ni moja ya nyuga muhimu za kuhamasisha usomaji katika jamii na hatimaye kujiletea maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kielimu. Makala haya yanajadili dhima ya muziki huu katika kuhamasisha usomaji katika jamii. Katika mjadala wetu masuala mbalimbali yanagusiwa kama vile lugha, elimu, utandawazi, utamaduni, vyombo vya habari na matamasha ya muziki. Makala yanahitimisha kuwa usomaji huo katika wakati wetu wa sasa unaimarika sana kwa wasanii na jamii kifani na kimaudhui kupitia muziki huu wa kizazi kipya.

## 1.0 Utangulizi

*Hip hip* na Bongo Fleva, maarufu kama muziki wa kizazi kipya, ni muziki ambao hufanywa sana na vijana nchini Tanzania. Muziki anzilishi wa Bongo Fleva au muziki wa kizazi kipya ni *Hip hop* au *rap*. Muziki huu ulianza kushamiri nchini Tanzania kuanzia miaka ya 1980. Hata hivyo, jitihada zinafanywa na baadhi ya wasanii kuunasua muziki wa *Hip hop/rap* kutoka katika kapu la Bongo Fleva kwa madai kuwa muziki huu upo ndani ya utamaduni wa *Hip hop* wenye misingi yake.

Akizungumzia muziki wa *Hip hop* nchini Marekani Rose (1994) anaeleza kuwa muziki huu ulianzishwa hasa na vijana wa Kimarekani na Kikaribiani wenye asili ya Kiafrika mnamo miaka ya 1970 katika jiji la New York. Kukosekana kwa huduma muhimu, maisha duni, ukandamizaji, umaskini kuliwafanya vijana hawa watafute njia ya kuelezea matatizo yao. Hivyo muziki wa *Hip hop* au *rap* ukaanza miongoni mwa vijana hawa maskini ili kuelezea matatizo yao na kuwawakilisha Wamarekani weusi wenzao. Vijana hawa waliokuwa wakidai haki walianzisha utamaduni wa *Hip hop* ambao unaundwa na grafiti, yaani maandishi ya ukutani, mavazi, lugha na muziki wa *rap* ili kuleta umoja na utambulisho wao (Rose, 1994). Kwa upande wake, akizungumzia muziki pendwa na muziki wa watu weusi nchini Marekani Roach (1992: 318) anasema kuwa ingawa ni vigumu kufasili muziki wa watu weusi, muziki wa *rap* unawakilisha Wamarekani weusi ambao asili yao ni Afrika. Makala haya pia yanaona kuwa asili ya muziki wa *rap* ni Afrika kutokana na sifa zake mbalimbali za kishairi na kiutamaduni ikiwemo vionjo vya kifani na vya kiutendaji vya kifasihi simulizi.

Miaka ya 1980 muziki na utamaduni wa *rap* ulianza kuingia na kuenea Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo. Hii ilitokana na kukua kwa athari za utandawazi na kukua kwa sayansi na teknolojia ambako kulirahisisha kurekodi muziki bila ya hata ya msanii kuwa na taaluma rasmi ya muziki. Halikadhalika, kuanzishwa rasmi kwa uchumi huria nchini Tanzania miaka ya 1980 kulichapusha uingizaji huria wa bidhaa mbalimbali zikiwemo kanda za muziki. Vijana wa Kitanzania walioenda ughaibuni kimasomo au kutembelea jamaa zao waliporudi nchini walileta kanda au DIGA (CD) za muziki wa *Hip hop*. Pia, waliweza kuona na kujifunza *Hip hop* kupitia sinema za Hollwood. Muziki wa Hip hop ulipoingia Tanzania uliimbwa kwa Kiingereza kwa sababu wasanii waliiga moja kwa moja nyimbo za *Hip hop* za Kamarekani (taz. Remes, 1998; Haas and Gesthuizen, 2000; Perullo 2003; Mangesho, 2003; Omari, 2009). Raghba na ubunifu wa kutaka kuimba kwa Kiswahili kulisababisha vijana wengi, ikiwemo na wale wasiojua Kiingereza na wenye utetezi wa Kiswahili, kuanza kuingia katika muziki huu kwa wingi. Kukua na kuendelea kwa muziki huu kibunifu na katika vionjo vyake vya kifashi, kimuziki na utamaduni kutoka ndani na nje ya Tanzania pamoja na matumizi makubwa ya Kiswahili miongoni mwa wasanii wake kulihalalisha kuuita muziki huu Bongo Fleva.

## 2.0 Dhima ya Muziki wa Bongo Fleva katika Usomaji

Makala haya yanaangalia usomaji katika maana pana, yanaona kuwa usomaji si tu uwezo wa kuelewa kusoma na kuandika (taz. Goody na Watt, 1968) bali ni pamoja na uwezo wa kuelewa maandishi na yale ambayo hayamo katika maandishi. Lengo la makala haya ni kuchambua mchango wa nyimbo za muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva kama sanaa muhimu katika kuwasiliana, kuwajuza wasanii na kuijuza jamii kuhusu mambo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Makala haya pia yataangalia baadhi ya vipengele vya kifani, kiutamaduni na kimaudhui vya muziki wa Bongo Fleva na dhima zake katika usomaji. Dhima ya usomaji katika muziki wa Bongo Fleva inajitokeza kama ifuatavyo:


### 2.1 *Hip hop* na Bongo Fleva na Dhima ya Kifasihi na Kiutamaduni

Muziki wa Bongo Fleva una mchango mkubwa kwa jamii na wadau wake mbalimbali: wasanii wenyewe, mapromota, madijei, wasambazaji, wauzaji, wasikilizaji na jamii kwa ujumla. Kwa upande wa fasihi, mashairi ya muziki huu hayako nyuma katika kuburudisha na kuelimisha kuhusu mambo mbalimbali kama vile uchumi, siasa na utamaduni. Wasanii wengi wa *Hip hop* na Bongo Fleva nchini Tanzania, kama walivyo wasanii wengi wa muziki wa *Hip hop* ulimwenguni kote, wana mchango mkubwa kama walimu katika kujuza, kuelewesha na kuelimisha mambo mbalimbali katika jamii zao (taz. Perullo, 2003; Reuster-Jahn, 2007; Suriano, 2007; Omari, 2009; Samwel, 2012).

Suala hili linadhihirishwa na Msanii Happiness Thadeo, anayejulikana kwa jina la kisanii kama Sister P katika wimbo wake uitwao DJs:

> Kwanza naanza na DJs kuweni makini...
> Tungo zako sharti ujumbe zibebe
> Zielimishe jamii ile utakacho waelewe
> Tungo zako zikubalike zitumike hata kwenye mashule
> Hili ndilo darasa nakupa *Hip hop* shule
> *Hip hop* nguzo ya tano michoro

Sister P anawaasa wasanii wenzake kuwa nyimbo za *Hip hop* na Bongo Fleva zinapaswa kubeba ujumbe ili ziweze kukubalika na jamii na kutumika hata shuleni. Anaendelea kusema kuwa grafiti au michoro inayochorwa sehemu mbalimbali, kama nguzo mojawapo ya utamaduni wa *Hip hop*, zina nafasi kubwa katika jamii hivyo zinapaswa kuzingatiwa na hadhira. Waandishi wa grafiti hawana budi kuandika mambo ya maana kwani *Hip hop* inaongea masuala muhimu ikiwemo ukweli kama mchoro huu hapa unavyosema:




Grafiti: '*Hip hop inaongea ukweli*' katika masikani ya Kikosi cha Mizinga, Kinondoni, Dar es Salaam (picha na mwandishi, 2005).

Ingawa wadau wakubwa wa muziki huu wanaonekana kuwa ni vijana lakini nyimbo zake zinasikilizwa na rika zote, vijana kwa wazee. Nyimbo na utamaduni unaoambatana na wasanii wengi wa *Hip hop* na Bongo Fleva kama vile mavazi (wanaume kuvaa hereni, kuvaa fulana kubwa, suruali kuvalia

makalioni) na lugha (matumizi makubwa ya misimu na lugha ya mtaani) yanasaidia kuyaelewa maisha na utamaduni wa vijana wa sasa duniani kote. Kwani usomaji, *kama ilivyo Bongo Fleva*, hutusaidia kujua mambo mbalimbali ya jamii na pia kwenda na wakati na mabadiliko mbalimbali duniani (Nsibambi, 2000:2, msisitizo ni wangu). Kama Afrika Bambaata (1996) anavyofasili 'utamaduni wa *Hip hop* kuwa unajumuisha mambo mbalimbali kama vile mavazi, matendo, jinsi unavyoonekana na jinsi unavyoongea, lugha yote haya hufanya utamaduni wa *Hip hop* [1]'.

Hivyo basi, muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva hutumika unaakisi masuala mbalimbali nchini kama zilivyo kazi nyingine za kifasihi kama vile riwaya na tamthiliya na aina nyingine za sanaa kama vile taarabu, dansi na ngoma. Mashairi ya muziki huu ni matini muhimu za kifasihi ambazo zimesheheni fani na ujumbe lukuki. Halikadhalika, wasanii wa Bongo Fleva wanatumia vionjo mbalimbali vya kisanaa. Matumizi ya vionjo hivi vya kifasihi na kiutamaduni huufanya muziki huu kupendwa. Vionjo hivi pia hukuza, huendeleza na huthamini amali za kifasihi na kiutamaduni za Kiafrika. Baadhi ya mbinu hizo kutoka katika fasihi simulizi ya Kiafrika, ikiwemo Tanzania, ambazo hutumiwa na wasanii katika muziki huu ni majigambo, nyimbo za watoto, utani, utambaji wa vitendawili na usimulizi wa kihadithi.

Halikadhalika, mashindano miongoni mwa wasanii wa muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva huzidi kumkuza na kumuendeleza msanii kisanaa na kimuziki kwa ujumla. Kuwepo kwa mashindano ambayo pia huwashirikisha wasanii wa *Hip hop* na Bongo Fleva kama vile *Kill Music Awards*, Mkali wa Rhymes (lilikwishafutwa) na *Bongo Star Search* huwasaidia wasanii kuwa makini katika utunzi au ubunifu wa nyimbo zao ili waweze kushindanisha tungo zao na za wasanii wengine. Vilevile, matamasha na ziara za wasanii nchini hufanya jamii kujifunza (ujumbe, utamaduni na lugha) kutoka kwa wasanii hawa. Vilevile kualikwa kwa wasanii wa Kitanzania nje ya nchi huhamasisha wasanii kujifunza masuala ya msingi kama vile lugha na utamaduni wa jamii au nchi waitembeleayo. Kwa kufanya hivyo hupanua uelewa wa msanii pamoja na hadhira katika masuala mbalimbali.

### 2.2 Lugha ya *Hip hop* na Bongo Fleva na Uhamasishaji Usomaji

Kama tulivyosema mwanzoni kuwa lugha waitumiayo wasanii wa muziki huu nchini Tanzania kwa sasa katika nyimbo zao ni Kiswahili. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kueleweka kwa lugha ya Kiswahili na walio wengi na ndiyo lugha ya taifa ya Tanzania. Matumizi ya Kiswahili katika muziki wao

---

[1] http://www.daveyd.com/whatisbam.html

kumefanya vijana kutoa na kueleweka mawazo yao kiurahisi. Kwani lugha asilia humtambulisha mtu kiutamaduni na humfanya kujieleza kwa urahisi. Pia, yamesaidia uhuru wa kubuni na kutoa mawazo mapya, hivyo kufikisha ujumbe wao kwa hadhira ipasavayo. Ingawa kuna matumizi makubwa ya Kiswahili wasanii wa *Hip hop* na Bongo Fleva pia huchanganya na lugha nyingine za kigeni na kienyeji ili kuleta ujumi wa kisanaa, kufikisha ujumbe na kutambua nafasi ya lugha nyingine katika mawasiliano. Jambo ambalo pia lilitiliwa mkazo na wanafasihi na washairi maarufu wa ushairi wa Kiswahili Tanzania kama vile Shaaban Robert katika kazi zake. Shairi lake la 'Kila Lugha' katika *Mwafrika Aimba* (1969:34) ubeti wa 7 anasema:

> Lugha ngeni ninakiri zina manufaa kwetu,
> Tujifunze kwa dhamiri, tuseme kama upatu,
> Walakini tufikiri, ubora wa lugha yetu,
> Hima pakutane watu au tutahasiri.

Uchanganyaji wa lugha katika nyimbo za Bongo Fleva ni mbinu mojawapo ya kuongeza ujumi katika kazi zao na kutambua umuhimu wa kila lugha duniani.

Halikadhalika, muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva una matumizi lukuki ya misimu. Matumizi ya misimu katika muziki huu huufanya kueleweka na wadau wengi wa nyimbo hizi, hasa vijana wenyewe. Baadhi ya misimu hiyo kama vile *beef* (ugomvi) na *blunt* (bangi) imetoka katika lugha ya Kiingereza. Ili msanii aweze kuitumia misimu hiyo katika nyimbo zake hana budi kujifunza na kujua maana yake kwanza kutoka lugha chanzi. Msanii hulazimika kusikiliza nyimbo mbalimbali za wasanii wa nje, kusoma magazeti, kutembelea tovuti mbalimbali na kuwasiliana na wasanii wengine ili kuweza kujenga ufahamu wa mambo kadha wa kadha. Kiessling and Mous (2004: 314) wanaeleza kwa usahihi:

> *To speak the youth language well means to be aware of the latest norms.*
> [kusema lugha ya vijana vizuri inabidi kujua mitindo itokeayo sasa (tafsiri yetu)].

Kiitikio cha wimbo uitwao 'Mikasi' wa msanii Albert Ngwair akimshirikisha Ferooz Mrisho unatudokeza juu ya utumiaji wa misimu katika nyimbo zao:

> Mitungi, *blunt*, mikasi
> Kama unataka kuvinjari nasi
> Mfukoni mambo yako yawe safi

Katika kipande hiki cha wimbo kuna matumizi ya misimu kama vile mitungi kumaanisha pombe, *blunt* (bangi) na mikasi (kufanya mapenzi). Wimbo huu si tu unatuonesha mambo ambayo vijana hawa wanayafurahia wakati wa

kujivinjari bali matumizi yao ya lugha ni hazina kubwa kwa masuala ya utafiti. Halikadhalika, misimu hii ambayo hutoka ndani na nje ya nchi inapopata mashiko husaidia katika kukuza msamiati wa lugha husika.

Aidha, matini za nyimbo za *Hip hop* na Bongo Fleva zimejaa matumizi ya lugha ya picha, kejeli na tamathali mbalimbali za semi. Wakizungumzia sifa za mshairi wa majigambo, hasa umilisi wa lugha kisanaa na maarifa kwa ujumla, Vail na White (1991: 77) wanasema:

> *The poet is expected to be eloquent, someone who can speak well. But he is above all expected to be knowledgeable.*
> [Mshairi anatarajiwa kuwa mahiri, mtu ambaye anaweza kuzungumza vizuri. Lakini zaidi ya yote anatarajiwa kuwa mjuzi wa mambo [Tafsiri yetu].

Hivyo basi katika kuzungumzia masuala mbalimbali katika nyimbo zao wasanii wa muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva wanapaswa kuelewa mambo mbalimbali ndani na nje ya jamii zao. Hii ni pamoja na masuala ya historia, siasa, uchumi, na kadhalika. Mambo ambayo humpasa msanii asome na kujua mambo mbalimbali ya jamii yake, ajue wasanii wa ndani na nje na ubunifu wa kisanaa, hivyo kuzidi kujiongezea maarifa siku hadi siku. Hivyo mbali na kutoa elimu kwa jamii wasanii pia hujielimisha, kwani ili kubobea katika utunzi ni vema kujua kazi za wasanii wengine na mambo mengine mengi. Ujuzi wa lugha mbalimbali hurahisisha jambo hili. Kwani matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha humpa msanii elimu, burudani na umilisi wa lugha katika kujieleza, umahiri katika utunzi wa kazi zake na uwezo wa kiuhakiki wa kazi za wasanii wenzake. Matumizi ya lugha kisanaa ni njia nzuri katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Mathalan, nyimbo kama za Profesa Jay, Sugu, Wagosi wa Kaya, Afande Sele, Zay B, G Solo, Lady Jaydee, TMK Wanaume, Ambwene Yessaya, Mwanafalsafa na wengineo zimesheheni maudhui lukuki kuhusu UKIMWI, siasa, masuala ya wanawake, rushwa, haki na vionjo mbalimbali vya lugha.

### 2.3 *Hip hop* na Bongo Fleva Hukuza Stadi za Lugha na Mawasiliano

Tunapozungumzia stadi za lugha kimsingi tunamaanisha kuzungumza, kusikiliza, kuandika na kusoma. Bongo Fleva inawasaidia wasanii katika kukuza stadi hizi. Na hili linajidhihirisha katika nyimbo zao kwa jinsi wanavyoimba haraka kiasi hata cha mtu wakati mwingine kushindwa kusikia au kuelewa wanasema nini. Msanii Yesaya Ambwene (AY) ni miongoni mwa wasanii wanaoimba haraka. Kushiriki katika muziki huu pia huwapa wasanii nafasi ya kujizoeza kusoma machapisho, tovuti na kazi mbalimbali za wasanii wengine na utamaduni wa *Hip hop* kwa ujumla. Halikadhalika, huwajengea ujuzi wa kuandika wakati wa utunzi wa nyimbo zao. Hivyo hata wale vijana

ambao hawakubahatika kuingia katika mfumo rasmi wa elimu inabidi wajifunze kuandika ili waweze kuandika wenyewe mashairi ya nyimbo zao.

Kwa wale waliosoma shule na kushindwa kuendelea na masomo ya juu kutokana na sababu mbalimbali muziki huu pia unawafanya wazidi kujiendeleza. Wasanii wengine hupata hamu ya kusoma masuala ya muziki baada ya kuwa wameshajiingiza kwanza katika uimbaji wa muziki huu. Halikadhalika, ili kutunga na kuandika mashairi ya Bongo Fleva inabidi msanii ajifunze au asikilize kazi mbalimbali za wasanii wengine. Kama Camita (1997:238) anavyosema kuwa ingawa nyimbo za *rap* huwasilishwa kwa mdomo kwa kufuata mapigo ya muziki lakini hutungwa kwanza kwa kusawiri mashairi na hata kusoma mashairi ya wasanii mahiri. Amri Abedi katika kitabu cha *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954) pia anasisitiza kuwa mojawapo ya sifa ya utunzi mzuri wa mashairi ni pamoja na kujizoeza kusoma kazi nyingi za washairi wengine na hasa wabobevu.

Tofauti na muziki wa dansi na taarab nchini Tanzania, sanaa ya *Hip hop* na Bongo Fleva imesababisha wasanii kwa kiasi kikubwa kuchanganya lugha au kubadili msimbo, hasa Kiswahili na Kiingereza. Suala hili kwa msanii si baya kisanii na kimaendeleo kwa ujumla, katika kujifunza na kutambua nafasi ya lugha nyingine, kwani kwa kufanya hivyo msanii hujifunza na kutumia lugha nyingine. Halikadhalika, mitindo ya lugha ya vijana wa mijini Afrika inasaidia kuunda utambulisho mpya miongoni mwao. Kubadili msimbo ni moja ya mbinu maarufu miongoni mwa vijana katika miji mbalimbali Afrika (Kiessling na Mous, 2004). Mtindo wa kubadili msimbo katika nyimbo zao, hasa Kiswahili na Kiingereza, hupendwa na wasanii wengi wa muziki huu. Hali hii uhamasisha baadhi ya wasanii kutaka kujifunza lugha za kigeni au maneno fulani ya lugha ihusikayo. Wasanii wa muziki wa *Hip hop* nchini hujenga ari ya kujifunza lugha na/au utamaduni wa fani husika kutoka mataifa ya Ulaya na Marekani kila wakati ili kuimarisha utunzi wa nyimbo zao. Wasanii pia hujifunza mitindo mbalimbali ya uandishi wa grafiti kutoka kwa wasanii wenzao. Grafiti, ambazo huwa wanazichora katika kuta za maskani yao, zina ustadi na ubunifu mkubwa.

### 2.4 *Hip hop* na Bongo Fleva katika Uhamasishaji Elimu

Kama tulivyokwishasema hapo awali, utungaji wa nyimbo za *Hip hop* na Bongo Fleva uliwakuza vijana kiakili kwani ujuzi wa kusoma na kuandika huanza na uwezo wa kuzungumza. Mbali na kutunga nyimbo wasanii hawa huchambua mambo mbalimbali ambayo yanawahusu vijana kama vile ukosefu wa ajira, utamaduni na jamii kwa ujumla. Kwa kuwa watunzi ni vijana wenyewe hivyo nyimbo zao zina mambo mengi ambayo yanawahusu. Hivyo baadhi ya mashairi ya *Hip hop* na Bongo Fleva yanaweza kutumika shuleni

kuchambua mambo mbalimbali na kama kiungo kati ya fasihi pendwa na fasihi ya dhati. Kwani katika muziki huu tunaweza kupata kila ujumbe tuutakao kama vile siasa, uchumi, afya na utamaduni. Kutokana na mchango na dhima ya muziki huu katika jamii yetu ya sasa haina budi vipengele vyake vifundishwe shuleni ili kujenga ubunifu miongoni mwa wanafunzi na kutambua mchango wake kwa jamii kwa ujumla. Halikadhalika, Mangesho (2003:161) anafafanua kuwa utamaduni wa Bongo Fleva unaweza kuwa muhimu sana kwa watoto kwani ni kama mfumo wa elimu kwa kuwa wanafunzi wanasikiliza zaidi muziki kuliko kile wanachofundishwa darasani.

Mathalan, katika masomo ya fasihi, utamaduni, muziki na lugha wanafunzi wanaweza kujifunza kupitia muziki huu. Kuna umuhimu mkubwa wa muziki huu kukuza na kuendeleza usomaji mashuleni; kwa hakika wanafunzi watafurahia sana. Utamaduni pendwa humfanya mwanafunzi kuunganisha usomaji wa shuleni na wa nje ya shule. Hii humvutia mwanafunzi katika kujifunza kwa kuakisi mambo yanayomhusu na humjengea ubunifu (Marsh na Millard, 2000; Hill 2007). Mathalan, kujifunza utunzi wa nyimbo za *Hip hop* kutamfanya mwanafunzi kutoogopa kujifunza ushairi. Hii ni kutokana na dhana iliyojengeka kwa baadhi ya watu kwamba ushairi ni mgumu (taz. Cooks, 1980 katika Kafeero, 2000). Hivyo itamfanya mwanafunzi kujenga misingi ya utunzi na uchambuzi wa ushairi tangu mapema. Wanafunzi watajifunza ushairi mapema kwa kuanza na ule waupendao na wausikiao kila siku. Hii itawafanya kuelewa kuwa kila mtu anaweza kuwa mtunzi wa ushairi. Kufundisha muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva na utamaduni wake shuleni kutasaidia kuakisi maisha ya wanafunzi na vijana kwa ujumla kwa sasa. Pia, kutasaidia kuendeleza usomaji na kuwajengea vijana utambuzi na uhakiki wa masuala mbalimbali ya jamii. Muziki huu una nafasi kubwa katika jamii, utamaduni, taaluma na utafiti.

Baadhi ya nyimbo za *rap* zinaweza kutumika darasani kutokana na ujumbe wake katika masuala mbalimbali kama vile elimu, utamaduni, na siasa. Muziki wa *rap* umekuwa ukitumika shuleni katika nchi nyingine kama vile Marekani (Lee, 1993; Mahiri, 1998; na Brown 2005) kwani unawasaidia wanafunzi kuandika, kuchambua, kuhakiki fasihi hiyo na hata masuala mengine. Uchambuzi wa vipengele mbalimbali vya kifani, kimuziki na kimaudhui utaanza kumjenga mwanafunzi juu ya nafasi ya muziki huu katika jamii yake. Tafiti zinaonesha kuwa matumizi ya *Hip hop* darasani yana umuhimu ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wanafunzi ambao hawana raghba ya kujifunza kuandika. Hivyo huchochea uandishi miongoni mwa wanafunzi (Lee, 1993; Mahiri, 1998; Brown, 2005). Lengo kuu ni kuendeleza na kuimarisha wanafunzi kupata na kushiriki usomaji wa kitaaluma (Morrell na Duncan-Andrade, 2002; Rice, 2002). Kimsingi, wasanii wengi pia huwa na matarajio kuwa kazi zao

zitatumika katika taasisi za elimu. Englert (2008: 48) katika mahojiano yake na Peter maarufu kama Chief Kiwinga pia anathibitisha jambo hili:

> Wasanii wengi maandagraundi (wachanga) *na wa muda mrefu* hulenga kuelimisha jamii kupitia muziki wao...Kutokuwa na elimu rasmi sio kikwazo kwa wao kutotimiza lengo hili katika jamii...Mimi kama msanii natakiwa nitoe ufahamu wangu. Ule ufahamu wangu jamii iupokee. Na inawezekana mashairi yangu yatumike mpaka kwenye mashule. Hilo ndiyo lengo kuu (msisitizo wetu).

Kwa hakika matarajio ya kutumika nyimbo zao shuleni yapo kwa wasanii wachanga na wabobevu. Kupigwa kwa wingi kwa muziki huu katika redio na televisheni husaidia kufikisha ujumbe kwa hadhira kwa wanaojua na wasiojua kusoma (taz. Perullo, 2005:77). Matumizi ya nyimbo hizi shuleni kutafanya ujifunzaji kuwa la kuvutia.

### 2.5 *Hip hop* na Bongo Fleva na Ukombozi wa Kijamii na Kiuchumi

Mnamo miaka ya 1990 wakati *Hip hop* inashamiri nchini Tanzania, ilionekana kuwa ni muziki wa kihuni hivyo baadhi ya wazazi waliwakataza watoto wao kujihusisha nao. Hii ni kutokana na kwamba uliambatana na matumizi ya uvutaji au kusifia bangi na maadili ambayo yalionekana kuwa ya kigeni. Wazazi hawakujua kuwa vijana daima wako mstari wa mbele katika kujijuza mambo mbalimbali yatokeayo miongoni mwa vijana wenzao ulimwenguni kote ili pia wawajuze wenzao kama Camita (1997:232) anavyosema:

> *Being part of the literate adolescent community meant being a reader/editor of adolescent literature. Adolescents collect their own texts and those of the other adolescents. They also collected texts from magazines, newspapres, texbooks, websites, etc.*
>
> [Kuwa miongoni mwa jamii ya vijalunga wasomi inamaanisha kuwa msomaji/mhariri wa fasihi ya vijana. Vijana hutafuta matini zinazowahusu na zinazowahusu vijana wenzao. Pia hukusanya matini kutoka katika majarida, magazeti, vitabu, na tovuti (Tafsiri yangu) ili kujifunza zaidi na kuwajuza wengine].

Kwa sasa ni dhahiri kuwa muziki huu si uhuni tena kwani umuhimu wake mkubwa si tu kwa wasanii wenyewe bali kwa watengenezaji (maprodyuza) na wasambazaji, Wamachinga, wazazi na jamii kwa ujumla. Muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva unatazamwa kama chombo muhimu cha kujikomboa kiuchumi na kisiasa miongoni mwa wasanii wake na jamii kwa ujumla. Muziki huu umekuwa ni miongoni mwa vyombo muhimu vya kutolea elimu kwa jamii kama vile masuala ya afya, elimu, uchumi, utamaduni na siasa. Pia, umeleta maendeleo endelevu kwa vijana, kwani vijana wengi wanaojishughulisha na muziki huu ni wale ambao hawana elimu ya juu lakini wameweza kumudu na kujiendeleza kimaisha kutokana na kufanya muziki huu. Hivyo, baadhi yao kujikwamua kutokana na tatizo la ajira ambalo linawakumba vijana wengi.

Baadhi yao wameweza kujenga nyumba, kununua magari na kufungua studio zao za kurekodia muziki. Hivyo imewafanya wasanii kujiendeleza kimaisha na kielimu, na hivyo kujikomboa kiuchumi. Ubunifu na utunzi mzuri wa baadhi ya nyimbo zao huwafanya watu kununua nyimbo hizo na kuhudhuria matamasha yao na kuwaletea maendeleo ya kimuziki na kiuchumi.

**3.0 Hitimisho**

Makala haya yamejadili dhima ya muziki wa muziki wa *Hip hop* na Bongo Fleva katika kuhamasisha usomaji kwa maendeleo ya wasanii, vijana na jamii kwa ujumla. Ingawa baadhi ya tamaduni za muziki huu zinalaumiwa kwa baadhi ya wasanii wake kujihusisha na uvutaji bangi na migogoro lakini kwa upande wa pili una nafasi muhimu katika jamii. Makala haya yamejadili kuwa *Hip hop* na Bongo Fleva ni chombo muhimu katika kupata habari mbalimbali zenye faida kwa msanii na jamii yake kwa ujumla na kuhamasisha usomaji. Jamii haina budi kufuatilia utamaduni wa vijana kupitia *Hip hop* na Bongo Fleva.

## Marejeleo


Abedi, A. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Brown, A. F. (2005). "Using Hip-Hop in Schools: Are We Appreciating Culture or Raping Rap? (The Council Chronicle, Nov. 05)". National Council of Teachers of English. Urbana, Illinois.

Camita, M. (1997). "Vernacular Writing: Variety of Literacy Among Philadelphia High School Students". *Cross-Cultural Approaches to Literacy*. Brian Street (ed). Cambridge: Cambridge University Press

Cooks, J. (2004). "Writing for Something: Essays, Raps, and Writing Preferences." *English Journal,* Sept. 2004; 94, 1, 76–77.

Englert, Birgit (2008). "Kuchanganyachanganya - topic and language choices in Tanzanian youth culture", *Journal of African Cultural Studies*, 20: 1, 45 — 55

Goody, J. and Watt, I. (1968). 'The consequences of literacy' in *Literacy in Traditional Societies*, J. Goody (ed.), 27–68. Cambridge/New York: Cambridge University Press.

Haas, P. J and Gesthuizen, T. (2000), "Ndani ya Bongo: Kiswahili Rap Keeping it Real", in Gunderson, F. and Barz, G. (eds.). *Mashindano! Competitive MusicPerformance in East Africa*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Hill, M. L. (2007). "Toward a Pedagogy of the Popular: Bourdieu, hip-hop and out-of-school literacies". *Pierre Bourdieu and Literacy*. James Albright and Allan Luke (eds.). Cambridge University Press. Pp 136-161.

Kafeero, I. (2000). "Mother Tongue Poetry and the Appreciation of Poetry in English". *Language and Literacy in Uganda: Towards a Sustainable Reading Culture*. Kate Parry (ed.). Kampala: Fountain Publishers, 92-96.

Kirkland, D.E. (2008). "You Must Learn": Promoting Hip-hop in Education. http://www.youthmediareporter.org/2008/06/you_must_learn_promoting_hipho

Lee, C.D. (1993). *Signifying as a Scaffold for Literary Interpretation: The Pedagogical Implications for an African American Discourse Genre.* Urbana, Ill.: National Council of Teachers of English.

Mahiri, Jabari. (1998) *Shooting for Excellence: African American and Youth Culture in New Century Schools.* New York: Teachers College Press.

Mangesho, P. (2003), "Global Cultural Trends: The Case of Hip hop Music in Dar esSalaam", *Unpublished MA Dissertation*, University of Dar es Salaam.

Marsh, J. Na Millard, E. (2000). *Literacy and Popular Culture: Using Children's Culture in the Classroom*. London: Paul Chapman.

Morrell, E. & Duncan-Andrade, M.R. (2002). 'Toward a Critical Pedagogy of Popular Culture: Literacy Development among Urban Youth' *Journal of Adolescent and Adult Literacy.* 46, 72-77.

Morrell, E. & Duncan-Andrade, M.R. (2002). "Promoting Academic Literacy with Urban Youth through Engaging Hip-Hop Culture." *English Journal,* July 2002; 91 (6), 88–92.

Mwanjoka, Gerald. (2011). *Harakati za Bongo Fleva na Mapinduzi.* Dar es Salaam: Hakuna Mchapaji.

Newman, M. (2005). "Rap as Literacy: A Genre Analysis of Hip-Hop Ciphers." *Text* 25.3 399-436.

Nsibambi, A. (2000). Language and Literacy in Uganda: A view from the Ministry of Education and Sporsts. *Language and Literacy in Uganda: Towards a Sustainable Reading Culture*. Kate Parry (ed.). Kampala: Fountain Publishers.

Omari, S. (2009). Tanzanian Hip hop poetry as popular literature. Ph.D Thesis (Literature) University of Dar es Salaam

Perullo, A. (2003). The Life that I Live: Popular Music, Urban Practices, and Agency in Dar es Salaam, Tanzania. PhD Dissertation, Indiana University.

_______ (2005). Hooligans and Heroes: Youth Identity and Hip hop in Dar es Salaam, Tanzania. *Africa Today* 51(4)75-101. Indiana University Press.

Remes, P.W. (1998), "Karibu Geto Langu/Welcome in My Ghetto: Urban Youth,Popular Language and Culture in 1990s Tanzania", *Ph.D. Dissertation*,Northwestern University.

Reuster-Jahn, Uta. (2007). Let's go Party! Discourse and Self-Portrayal in the Bongo Fleva song

Mikasi ('Sex', Ngwair 2004). In: Swahili Forum. Vol. 14 (2007): 225-244. http://www.ifeas.uni-mainz.de/SwaFo/SF_14_13%20 Reuster-Jahn.

Rice, J.C. (2003). The 1963 Hip hop machine: Hip hop pedagogy as composition. College Composition and Communication, 54, 453-71.

Roach, H. (1992). *Black American Music: Past and Present.* 2nd edition. Malabar, Florida: Krieger Publishing Company.

Robert, S. (1969). *Mwafrika Aimba*. Nairobi: Nelson.

Rose, T. (1994). *Black Noise: Rap Music and Black Culture in Contemporary America.* New England: Wesleyan University Press.

Smitherman, G. (1997). "The Chain Remain the Same": Communicative Practices in the Hip-Hop Nation. *Journal of Black Studies, 28,* 1, 3--25.

Suriano, Maria. (2007). 'Mimi ni Msanii, Kioo cha Jamii'. Urban Youth Culture in Tanzania as seen through Bongo Flava and HipHop. In: Swahili Forum Vol. 14 (2007): 207-223. http://www.ifeas.uni-mainz.de/SwaFo/SF_14_12%20Suriano.pdf (last visited 15-04-2008).

**Diskografia**

Mangwair, Albert. (2003). *Mimi*. Dar es Salaam: GMC Wasanii Promoters.
Happiness Thadei. (2001). *Marekebisho*. Dar es Salaam: GMC Wasanii Promoters.